


KHAIR UL- BARIYAH

Kimeandikwa na:

**Jopo la wanavyuoni wa taasisi ya World Ahlul-Bayt
Islamic League (WABIL)**

Kimetarjumiwa na:

Dk. M. S. Kanju





ترجمة

خير البرية

تأليف

رابطة أهل البيت (ع) الإسلامية العالمية

من اللغة الإنكليزية إلى اللغة السواحلية



© **Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 512 - 72 - 0

Kimeandikwa na:

**Jopo la wanachuoni wa taasisi ya:
World Ahlul-Bayt (A.S) Islamic League (WABIL)**

Kimetarjumiwa na:

Dr. M. S. Kanju

Kimepangwa katika Kompyuta na:

Hajat Pili Rajab

Toleo la kwanza: Oktoba, 2011

Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info



NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kitiwacho, *Khayru 'l-Bariyyah* ambacho sisi tumekiita kwa jina hilohilo.

Jina la kitabu hiki linatokana na hadithi ya Mtukufu Mtume SAW kama ilivyosimuliwa na Ibn 'Asakir kutoka kwa Jabir bin Abdallah kwamba alisema: “Tulikuwa pamoja na Mtume SAW wakati Ali AS alipokuja (hapo tulipokuwa tumekaa). Mtume akasema: ‘Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake; hakika huyu (Ali) na Shia (wafuasi) wake ndio wenye kufuzu Siku ya Ufufuo.’ Kisha aya ifuatayo ikashushwa: *‘Hakika wale walioamini na kutenda mema, basi hao ndio wema wa viumbe!’*”¹

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

¹ Jalaluddin as-Suyuti (aliyekufa 910/1504-05), *ad-Durru 'l-Manthur*, jz. 6 uk. 379. Anasimulia hadithi kama hii kutoka kwa Ibn Abbas na Ali kadhalika katika sehemu hiyo hiyo; al-Khwarizini (aliyekufa 569/1173-4) katika *al-Manaqib*. Hadithi nyingine za Mtume SAW zitamkazo kwamba Shia wa Ali watafuzu siku ya Kiyama zinasimuliwa na muhadithina wa Kisunni kutoka kwa Abdullah, Abu Rafi', Jabir bin Abdullah, Ibn Abbas na Ali. Miongoni mwa muhadithina hao ni: at-Tabarani katika kitabu chake *al-Mu'jamu' l-Kabir*, Ahmad bin Hanbal katika *al-Manaqib*, Ibn Marduwayh na al-Kanji ash-Shafi'i (aliyekufa 658/1260) katika kitabu chake *Kifayatu 't-Talib* na wengine wengi.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Dk. M. S. Kanju kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni mwanga kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu ya dini na ya kijamii.

Mchapishaji:

Al-Itrah Foundation

S. L. P. 19701

Dar-es-Salaam.

Mpendwa msomaji.

Assalaam Alaykum Warahmatullah Wabarakatuh.

Kitabu hiki ni chapisho la Al-Itrah Foundation. Machapisho yake yameandaliwa ili kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi kwa kuzingatia msisitizo maalum wa kusafisha akili na fikra ya Mwislamu. Al-Itrah Foundation imefanya jitihada kubwa kuwasilisha kile tu ambacho ni Sahihi na cha kuaminika kwa mujibu wa Uislamu.

Tunakuomba ukisome kitabu hiki kwa dhamira iliyokusudiwa. Pia unaombwa ututumie maoni yako juu ya machapisho yetu, maoni ambayo sisi tutafurahi sana kuyapokea.

Kueneza ujumbe wa Uislamu ni kazi inayotaka ushirikiano wa watu wote. Al-Itrah Foundation inawaalikeneni kwenye kazi hii, ambayo ni mwitikio wa aya ya Qur'an isemayo:

﴿ قُلْ إِنَّمَا أَعْظَمُكُمْ بِوَاحِدَةٍ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مِثْلَىٰ وَفَرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُونَ ﴾

“Sema: Siwapatieni isipokuwa nasaha moja, kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kwa pamoja na mkiwa mmoja mmoja. (34:46).

**Mwenyezi Mungu Mtukufu awabariki!
Ndugu zenu katika Uislamu
Al-Itrah Foundation**



Khair-ul-Bariyyah

KHAIR-UL-BARIYYAH

﴿إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ هُم خَيْرُ الْبَرِيَّةِ﴾

Hakika wale walioamini na kutenda mema, hao ndio bora wa viumbe. (98:7)

1 Ghafila Mjumbe wa Allah (swt) alitamka:

“Ee Ali! Wewe unatokana na mimi, na mimi natokana na wewe.”²

2 Mus’ab Bin Sa’d anaandika kutoka kwa baba yake:

“Wakati Mtume wa Allah (swt) alipokuwa anataka kuondoka Madina kuelekea kwenye vita vya Tabuk, alimteua Ali (a.s.) kuwa kaimu Khalifa wake.

“Kwa kuachwa nyuma, Ali alilalamika: ‘Je, nikae nyumbani pamoja na wanawake na watoto?’ Mtume (saww) akasema kumwambia: ‘Je, huridhiki na ukweli kwamba wewe kwangu mimi ni kama alivyokuwa Harun kwa Musa, isipokuwa hakuna Mtume mwingine atakayekuja baada yangu?’”³

² *Sahih Bukhari*, Sura ya 10, uk. 580. Sura ya 14, uk. 386 na Sura ya 17, uk. 24; *Jam’a Tirmidhi* uk. 461; *Sunan Ibn Majah* uk.12; *Mishkat* Jz. 8, uk. 120 na uk. 128; *Mustadrak* Jz. 3, uk. 70; *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 257 na uk. 261; Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal* uk. 30 na uk. 447; *Kunuz-ul-Haqaique* uk. 20 na uk. 63; *Isabah* Jz. 4, uk. 271; *Riaz-un-Nazarah* Jz. 2, uk. 171; *Usd-ul-Ghaba* Jz. 4, uk. 27; *Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal* Jz. 1, uk.109 na 115, Jz. 5, uk. 204. Uk.356, uk. 358 na 359.

³ *Sahih Bukhari*, Sura 14, uk. 387 na Sura 18, uk. 89. *Sahih Muslim* Jz. 4, uk. 278. *Jam’a Tirmidhi* uk. 461, *Isabah* JZ. 4, uk. 270. *Usd-ul-Ghaba* JZ. 4, 25. *Izalatul Khifa Maqsad* JZ. 2, uk. 260. na 261. *Riaz-un-Nazrah*, JZ. 2, uk. 188 na uk. 203. *Musnad Imam Hanbal* JZ. 1, uk. 330. Dondoo kutoka *Kanz ul-Ummal*, uk. 53.

Khair-ul-Bariyyah

3 Mara nyingi Mtume (saww) alikuwa akitangaza:

“Ali kwangu mimi ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa.”⁴

4 Abu Huraira anasimulia:

“Mtume wa Allah (swt) alimuagiza Abu Bakr kutangaza katika Hija (ya mwaka wa 9 A.H.) kwamba mwaka huo haruhusiwi mushiriku yeyote kufanya ibada ya Hija mjini Makka, wala haruhusiwi yeyote kuzunguka Nyumba ya Allah (Al-Ka’abah) akiwa uchi.

“Kwa wakati huohuo, Mtume alimtuma Ali, akimuamuru kwamba yeye peke yake anatakiwa kuhubiri Sura ya Tawba (Sura ya 9 ya Qur’ani Tukufu).”

Abu Huraira akaongeza:

“Katika Siku ya Kuchinja alikuwa ni Ali ambaye alitoa tangazo miongoni mwa watu huko Mina kwamba mshirikina yeyote haruhusiwi kuhiji, wala mtu yeyote haruhusiwi kuizunguka Nyumba ya Allah (Al-Ka’abah) akiwa uchi.”⁵

5 Mtume (saww) alimtuma Abu Bakr, akimuamuru atangaze amri ya Allah, kwa niaba yake, mara Mtume (saww) akamtuma Ali.

⁴ *Sahih Bukhari*, Sura 14, uk. 387 na Sura 18, uk. 89. *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 278. *Sunan Ibn Majah* uk. 12. *Mishkat* JZ. 8, uk. 119. *Jam’a Saghir* uk. 56. *Kunuz-ul-Haqaique*, uk. 173. *Isabah* JZ. 4, uk. 25. *Riaz-un-Nazarah* JZ. 2, uk. 157; uk. 163; uk. 188 na uk. 203. *Mustadrak*, JZ. 2, uk. 337 na JZ. 3, uk. 19. *Isti’ab* JZ. 2, uk. 472. *Kanz-ul-Ummal* uk. 31 na uk. 370. *Izalat-ul-Khifa Maqsad* 2, uk. 260 na 261. *Musnad Imam Hanbal* JZ. 1, uk. 170, uk. 173, uk. 179, uk. 182, uk. 184 na 331, JZ. 3, uk. 32 na uk. 338, JZ. 6, uk. 369 na 438.

⁵ Tazama *Sahih Bukhari* Sura 2, uk. 238.

Khair-ul-Bariyyah

Abu Bakr alikuwa njiani akienda zake kama alivyotumwa wakati alipohisi kama vile aliyesikia ngamia wa Mtume akimpita, na alidhania kwamba Mtume wa Allah (swt) mwenyewe ndiye anayekuja. Lakini alipogeuka macho yake yaliangukia kwa Ali ambaye alimpa hati ya maandishi, inayosema Ali peke yake ndiye atangaze amri (hiyo) ya Allah.⁶

6 "...Huku akiwa amehuzunika Abu Bakr alirudi kwa Mjumbe wa Allah (swt) na akauliza iwapo kama ilikuwa ni amri ya Allah kwamba sura hiyo ya *Tawba* ichukuliwe kutoka kwake. Mtume (saww) akamwambia kwamba Allah amemuamuru kwamba tangazo la Sura hiyo lazima lifanywe na yeye mwenyewe (Mtume) au na mtu mwingine wa familia yake."⁷

7 "Ni dawa gani aliyopewa Mtume wakati alipojeruhiwa kule Uhud?" Baadhi ya watu walimuuliza Sahl Bin Sa'd Sa'adi. Sahl akajibu: "Ali alileta maji kutoka kwenye ngao yake, na Fatima alimsafisha kuondoa damu katika uso wake. Kisha ulichomwa mfuko na majivu yake yaka-jazwa kwenye jeraha."⁸

8 "...Katika giza nene wakati kila Sahaba amemkimbia Mtume (na kumuacha katika shida), Ali peke yake ndiye ambaye hakumkimbia."⁹

⁶ *Sahih Bukhari*, Sura 19, uk. 194. *Jam'a Tirmidhi* uk. 373. *Sunan Nasa'i*, JZ. 2, uk. 43.

⁷ *Khasais Nasa'i* uk. 14. *Kanz-ul-Ummal*, Sura 1, uk. 444. *Zalat-ul-Khifa Maqsad* 2, uk. 261. *Riaz-un-Nazarah* JZ. 2, uk. 203. *Isabah* JZ. 4, uk. 270.

⁸ *Sahih Bukhari*, Sura 1, uk. 176, Sura 11, uk. 88, Sura 12, uk. 122, Sura 16, uk. 148, Sura 23, uk. 407. *Musnad Imam Hanbal* JZ. 5, uk. 330.

⁹ *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 202. *Isti'ab* JZ. 2, uk. 470. *Izalatul-Khifa Maqsad* 2, uk. 261.

Khair-ul-Bariyyah

9 Usiku mmoja wakati wa vita vya Khaibar Mjumbe wa Allah (swt) alitabiri:

“Kesho asubuhi yule mtu shujaa atakabidhiwa Bendera, na katika mikono yake Allah ataleta ushindi. Na ambaye ana mapenzi makubwa kwa Allah na kwa Mtume Wake, na Allah na Mtume Wake pia humchukulia katika cheo kikubwa mno.” Kwa habari hizi, masahaba wote wa Mtume waliupitisha usiku huo katika shauku kubwa, waki fikiria ni nani huyo atakayetunukiwa heshima hiyo ya kukabidhiwa Bendara. Lakini Muhammad (saww) aliuliza: “Yuko wapi Ali?” wakajibu: “Anaumwa macho.” Hivyo Ali aliongozwa mpaka mbele ya Mtume. Mara moja Mtume akachukua mate mdomoni mwake na kuyaweka kwenye macho ya Ali, na maumivu yale yalitoweka kabisa kiasi kwamba ilionekena kama vile alikuwa haumwi macho. Kisha Muhammad akamkabidhi bendera. Na Ali akamuuliza: “Je, nikapigane nao mpaka wawe Waislamu kama sisi?”

“Kwanza fika kwenye sehemu ile na imani yote” Mtume wa Allah alimuamuru. “Na ukifika pale shuka chini na walinganie wote wawe Waislamu, ukiwaambia wajibu walionao kwa Allah kwamba ni wa lazima kwao. Kwani kama Allah atamwongoza yeyote miongoni mwao kwenye njia iliyonyooka kwa juhudi zako, ni bora kwako kuliko kutoa kundi la ngamia kama sadaka.”¹⁰

10 Masahaba wengi walinyanyua shingo zao juu ili Mtume wa Allah aweze kuwaona...”¹¹

¹⁰ *Sahih Bukhari*, Sura ya 12, uk. 96, uk. 106, na 114. Sura ya 14, uk. 386 na Sura ya 17, uk. 9.

¹¹ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 278 na uk. 279. *Jam'a Tirmidhi* uk. 461. *Mustadrak JZ.* 3, uk. 125. *Musnad Imam Hanbal JZ.* 2, uk. 26. *Tabaqat Ibn Sa'd JZ.* 2. *Qism* 1. *Isti'ab JZ.* 2, uk. 473. *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 187. *Isabah JZ.* 2, uk. 470. *Usd-ul-Ghaba JZ.* 21. *Kanz-ulUmmal* uk. 128 na uk. 130.

Khair-ul-Bariyyah

11 “Ni katika siku hiyo tu niliweka tamaa ya kuwa jenerali.” Alikiri Umar. “Wakati Mtume alipotangaza, ‘Kesho nitampa bendera mtu yule ambaye kutoka mikononi mwake Allah ataleta ushindi...’”¹²

12 Qais bin Ubadah anaandika, akiwa amaemsikia Ali akisema: “Siku ya Hukumu, nitakuwa mtu wa kwanza kuleta malalamiko yangu mbele ya Allah.”

Qais alieleza: “Sura ya 22, aya ya 19 ya Qur’ani Tukufu inasomeka: **‘Hawa mahasimu wawili waliohasimiana kwa ajili ya Mola wao...’**”

Iliteremshwa kuhusiana na wale ambao walipigana vita vya Badr, na walikuwa ni Ali, Hamza na Ubaida kwa upande mmoja, na Utba na Walid kwa upande mwingine.”¹³

13 Mtume wa Allah (swt) alitabiri kwa ajili ya Ali: “Wengine watapendelewa kuliko wewe wakati ambapo hawatakuwa katika haki zao wenyewe. Jitenge mwenyewe kwayo mpaka utakaponifikia katika Bwawa la Kauthar.”¹⁴

14 Mjumbe wa Allah (swt) alisema: “Kama mtamfanya Ali kuwa Khalifa wenu, ingawa najua hamtafanya hivyo, atawaongoza kwenye njia ya haki, na mtamuona kuwa ni kion-

¹² *Kanz-ul-Ummal* uk. 130.

¹³ *Sahih Bukhari* Sura 16, uk. 10 na 39. *Mustadrak*, JZ. 2, uk. 386. *Kanz-ul-Ummal* JZ. 1, uk. 462. *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 160. *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 265. *Tabaqat Ibn Sa’d* JZ. 2. *Qism* 1. uk. 2.

¹⁴ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 127.

Khair-ul-Bariyyah

gozi na mtu aliyeongozwa vizuri.”¹⁵

15. Mtume (saww) alisema:

“Kama mtamchagua Ali kuwa Amir wenu, ingawa najua hamtafanya hivyo, mtamuona kuwa ni kiongozi na mtu aliyeongozwa vizuri (kwa hilo). Atawaongoza kwenye njia iliyonyooka.”¹⁶

16. Hadhart Umar alitamka:

“Mtume (saww) alikufa katika hali ya akili wakati akiwa ameridhishwa vizuri na Ali.”¹⁷

17. Yazid Bin Habaan anaeleza:

“Hasiin Bin Samrah, Umar Bin Muslim na mimi tulimtembelea mzee (mwenye kuheshimiwa) Zaid Bin Arqam, sahaba wa Mtume (saww). Tulipokaa na kutulia, Hasiin alimuambia yule mzee: ‘Ewe Zaid! Unazo baraka nyingi (za Allah): umehudhuria hadhara za Mtume, umemsikia akisimulia hadithi, umepigana vita pamoja naye na umeswali nyuma yake. Hakuna shaka yoyote kwamba unazo baraka nyingi katika sifa yako. Ewe Zaid! Tusimulie sisi pia hadithi, kwani zako zilikuwa nyingi za kutosha ambazo umezisikia kutoka kwa Mtume wa Allah (swt).

“Zaid akasema: ‘Ewe mtoto wa ndugu yangu! Nimezeeka sana kwa hayo yote na pia ni muda mrefu mno. Hadithi nyingi ambazo

¹⁵ *Musnad Imam Hambal* kutoka kwenye dondoo za *Kanz-ul-Ummal* JZ. 1, uk. 29.

¹⁶ *Mishkat* JZ. 8, uk. 128. *Musnad Imam Hambal*, JZ. 1, uk. 109 na JZ. 5, uk. 356 na uk. 359. *Mustadrak* JZ. 3, uk. 70. (dondoo za) *Kanz-ul-Ummal* uk. 191. *Isabah*, JZ. 4, uk. 271. *Usd-ul-Ghaba* JZ. 4, uk. 31. *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 275, *Isti’ab*, JZ. 2, uk. 478.

¹⁷ *Sahih Bukhari* Sura ya 14, uk. 386.

Khair-ul-Bariyyah

nimezisikia kutoka kwa Mtume na kuwa na kumbukumbu nazo sasa zimetoweka kwenye kumbukumbu yangu. Hivyo tosheka na kiasi chochote kile ambacho nitaweza kukuambia, na tafadhali usisisitize mno juu ya yale yote ambayo siwezi kuyaeleza.’

“Baada ya kupumzika kidogo Zaid akaendelea kusema:

‘Siku moja Mtume alisimama ili atoe khutba kando ya chemchemu ambayo inaitwa kwa jina la Ghadir Khum na iko katikati ya Makka na Madina. Kwanza alimshukuru Allah, na akiwa amefanya mahubiri kutokana na hutuba yake hiyo, alianza kwa kusema:

‘Mimi pia ni mtu kama ninyi. Haitachukua muda mrefu mjumbe kutoka kwa Allah atanijia na itanibidi nikubali utashi Wake. Sikilizeni! Nakuachieni juu yenu vitu viwili vitukufu vyenye thamani, kimojawapo ni Kitabu cha Allah, ambacho kwacho mna mwongozo na mwanga kwa ajili yenu. Hivyo kishikilieni kwa nguvu zenu zote na shikamaneni nacho.’ Kisha Mtume (saww) akawafanya watu washikwe na shauku ya kuyatekeleza maelekezo yake na mwishowe akawaambia:

‘Kitu kingine kitukufu ni kizazi changu, Ahlu’l-Bayt wangu. Kuhusu Ahlu’l-Bayt wangu nawataka mumuogope Allah, katika kuwaheshimu Ahlu’l-Bayt wangu, nawatakeni ninyi mumuogope Allah.’”¹⁸

[18] Yazid Bin Habaan ananukuu kutoka kwa Zaid Bin Arqam:

“...Mtume (saww) alisema: ‘Nakuachieni vitu viwili vitukufu miongoni mwenu, kimojawapo ni Kitabu cha Allah, ambacho ni Kamba ya Allah. Mtu ambaye atashikilia kwayo atakuwa katika Njia iliyo

¹⁸ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 279.

Khair-ul-Bariyyah

Nyooka, na mtu ambaye anaacha kuishikilia atakuwa amepotea...”

Tulimuuliza Zaid Bin Arqam:

“Ni nani ambaye ni miongoni mwa kizazi? Hakika wake huunda familia!”

Zaid akajibu: “Hapana! Kwa jina la Allah, wake hawaishi na mume kwa muda mrefu. Isitoshe kama mke ametalikiwa, hurudi kwa baba na kwenye familia yake. Kizazi cha Mtume hutokana na jamaa zake wa karibu ambao, kama yeye, wanakatazwa kuchukua sadaka.”¹⁹

19. Barau Bin Aazib ananukuu kutoka kwa Zaid Bin Arqam, sahaba wa Mtume (saww):

“Akiwa njiani akirudi kutoka Hija yake ya mwisho, Mjumbe wa Allah aliwasili kwenye chemchem ya Ghadir, alishika mkono wa Ali na akawahutubia Waislamu (waliokuwepo pale), aliwauliza: ‘Je hamjui kwamba ninayo mamlaka makubwa juu ya maisha ya waumini kuliko walivyo wao wenyewe?’ hadhara yote ikajibu kwa pamoja: ‘Bila ya shaka (unayo), Ewe Mjumbe wa Allah!’ Mtume akauliza tena: ‘Je, mnajua kwamba nina ushawishi mkubwa juu ya maisha ya waumini na mamlaka juu yao kwa uimara zaidi kuliko walivyo wenyewe?’ wote wakajibu: ‘Hakika, kweli.’ Kisha Mtume (saww) akatamka: ‘Yeyote yule ambaye mimi ni mlezi wake, Ali vilevile ni mlezi wake. Allah na awe rafiki kwa yule ambaye ni rafiki wa Ali, na Awe adui kwa yule ambaye humfanyia uadui Ali.’

¹⁹ *Sahih Bukhari*, Sura ya 2, uk. 280. *Jam’a Tirmidhi* uk. 467 na uk. 468. *Jam’a Saghir* uk. 55. *Mustadrak JZ.* 3, uk. 148, na uk. 533. *Mishkat JZ.* 8, uk. 133. (dondoo za) *Kanz-ul-Ummal*, uk. 95. *Musnad Imam Hanbal*, JZ. 2, uk. 247, JZ. 3, uk. 14, uk. 17, uk. 26 na uk. 59. JZ. 4, uk. 367 na uk. 371. JZ. 5, uk. 182.

Khair-ul-Bariyyah

‘Mara baada ya tangazo hili alikuja Umar kumuona Ali na akatoa hongera zake, akasema: ‘Ewe Mtoto wa Abu Talib ubarikiwe. Kuanzia sasa na kuendelea umekuwa daima Bwana wa kila muumini mwanaume na mwanamke.’”²⁰

20 Zanzan Bin Umar, anaandika, akiwa amemsikia Ali akisema juu ya mimbari mjini Kufa akiwahutubia watu: “Yeyote yule ambaye alikuwa pamoja na Mtume (saww) pale Ghadir na kumsikia kwa masikio yake aliyoyasema pale, na asimame.”

Katika hili, Zanzan anaeleza, sio chini ya watu kumi na watatu walisisimama na kutoa ushahidi: “Tulimsikia Mtume pale Ghadir Khum akisema: ‘Yeyote yule ambaye mimi ni mlezi wake, Ali pia ni mlezi wake.’”²¹

21. Imenukuliwa kutoka kwa Tarique Bin Shaab:

‘Mmoja wa mayahudi alimwambia Umar: ‘Unasoma aya (5:67 na pia 5:3) kutoka kwenye Qur’ani ambayo ina maana sana kiasi kwamba kama ingeteremshwa kwetu, tungeitukuza siku hiyo ya kuteremshwa kwake kama Iddi ya kweli na uhakika.’

Umar akajibu: ‘Tunajua aya hiyo. Vilevile tunajua siku hiyo mahususi wakati ilipoteremshwa. Na pia, tunajua ni wapi alipokuwa wakati huo Mjumbe wa Allah. Aya hiyo ilishushwa Arafat ambako Mjumbe wa Allah alisimama.’”²²

²⁰ *Mishkat*, JZ. 8, uk. 120, uk. 122 na uk. 123. *Jam’a Saghir* uk. 154. *Kunuz-ul-Haqaique* uk. 13. *Mustadrak* JZ. 3, uk.109, uk. 110 na uk. 152, JZ. 4, uk. 368, uk. 370 na uk. 372. JZ. 5, uk. 347, uk. 366, uk. 370 na uk. 419.

²¹ *Musnad Imam Hanbal* JZ. 1, uk. 84 na uk. 88.

²² *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 419.

Khair-ul-Bariyyah

22 Hadharat Umar alitangaza:

“Nimepata kulifahamu hili pia kwamba mtu mmoja miongoni mwenu amesema kwamba wakati Umar akifariki atakula kiapo cha utii kwa fulani. Ama kwa hilo, lazima litamfanya mtu yeyote asiwe na shaka kudhania kwamba Ukhalifa wa Abu Bakr umetukia kwa mtindo wa ovyo ovyo au ni kitu ambacho kimeporwa. Kwa kusema kweli ulikuja kwa njia hiyo, lakini Allah aliunusuru usiangukie kwenye maangamizi.”²³

23 Hadharat Umar alimtembelea Ali na akamuuliza:

“Ewe Abul Hasan! Nieleze kwa jina la Allah kama kweli Mjumbe wa Allah alikufanya wewe kuwa Khalifa wake.” Ali akajibu: “Kama nikikuambia, ni jibu gani litakuwa kutoka kwa Bwana wako (Abu Bakr) na lako wewe mwenyewe?” Umar akajibu: “Ama kwa Bwana wangu hakuna tena zaidi, hakuna swali kutoka kwake, bali nazungumza kwa ajili yangu mwenyewe kwamba nitaliondoa jukumu la ukhalifa mabegani mwangu na kuliweka juu ya mabega yako.”

“Sasa hakuna suala kama hilo tena.” Alisema Ali, “nani atakayekuondoa katika ukhalifa? Lakini ukweli wa mambo ni kwamba Mjumbe wa Allah alinifanya mimi Nguzo ya Mwongozo, na kama mwenyewe nikijifanya kutetea madai yangu, mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na mimi atapotea.”²⁴

24 “Allah awasaidie,” Hadharat Umar aliomba kuhusu wajumbe wa Shura aliyoweka kuchagua Khalifa baada yake. “Kama watamchagua Ali kama Khalifa wao, ni yeye peke yake awezaye kuwaongoza kwenye Njia Iliyonyooka, kwa gharama yoyote, hata kama atakuwa

²³ *Sahih Bukhari*, Sura ya 28, uk. 368.

²⁴ *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 244.

Khair-ul-Bariyyah

ameshikiliwa kwa ncha ya upanga!”

“Kwanini usimteue wewe mwenyewe kuwa Khalifa, kama kweli ulikuwa na uhakika na Ali?” Msimuliaji (wa hadithi hii) alilalami-ka.²⁵

25 Ibn Abbas ananukuu:

“Wakati maradhi ya Mtume yalipozidi sana, aliomba aletewe kalamu na karatasi ili baada yake aache hati (ya maandishi) ambayo itawafanya watu wasipotee baada yake.” Lakini Umar mara moja akaingilia: ‘Mtume amezidiwa na maradhi. Kitabu cha Allah kinatocha (kutuongoza).’

Katika hatua hii, mfarakano ukajitokeza na mabishano yakawa makubwa. Hatimaye Mtume akasema: ‘Ondokeni! Mabishano na makelele sio sahihi mbele yangu.’” Wakati akiwa anaondoka Ibn Abbas akasema: “Ni Msiba mbaya kati ya misiba yote ambapo Mtume alizuiwa kuacha hati ya maandishi baada yake,”²⁶

26 Zahri ananukuu kutoka kwa Ubaidullah Ibn Abdullah ambaye alimsikia Hadharat Aisha akisema:

“Wakati Mtume wa Allah (swt) aliposhikwa na maradhi na maumivu yake yakawa makubwa, aliomba ruhusa kutoka kwa wake zake ili azitumie siku za maradhi yake nyumbani kwangu ambako atapatiwa

²⁵ *Riaz-un-Nazrah*, JZ. 2, uk. 242. *Istia'ab*, JZ. 2, uk. 485.

²⁶ *Sahih Bukhari*, Sura ya 1, uk. 106, Sura 12, uk.126, Sura 18, uk. 100, Sura 23, uk. 384, Sura 30, uk. 701. *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 43. Katika sura ya Jawaiz-ul-Wulud kitabu cha *Bukhari*, anumia maneno: ‘anaweweseka’ badala ya ‘amezidiwa na maradhi.’

Khair-ul-Bariyyah

huduma za uuguzi. Wakeze wote wakakubali ombi hilo. Katika siku hizo (za maradhi yake) alitoka nje akiwa amesaidiwa na watu wawili, na miguu yake ikiwa inaburuzika. Mmoja wa watu hao wawili ambao walijitolea kumsaidia Mtume ni Ibn Abbas na mtu mwingine.”

Ubaidullah anasema alilitamka hili kwa Ibn Abbas (mara moja) aka-niuliza: ‘Je, unajua mtu yule mwingine alikuwa nani ambaye Aisha aliacha kutaja jina lake?’ Ubaidullah akajibu: ‘Hapana simjui.’ Ibn Abbas akasema: ‘Alikuwa ni Ali Ibn Abi Talib.’”²⁷

27 Abdullah Ibn Zayd bin Asadi ananukuu:

“Wakati Talha, Zubair na Aisha walipokwenda Basra, Imamu Ali alimtuma Ammar Bin Yasir na Imam Hasan kwenda Kufa. Walipowasili huko, wote walikwenda kwenye mimbari, Hasan aka-panda ngazi ya juu ambapo Ammar alisimama kwenye ngazi ya chini. Sisi wote tulijikusanya mbele yao wakati nilipomsikia Ammar akise-ma: ‘Aisha amekwenda Basra. Ni kweli kwamba yeye ni mjane wa Mtume. Lakini Allah amekuwekeni katika mthani ili kujua iwapo mnamtii Yeye au mnamkubali Aisha.’”²⁸

28 Jabir Bin Samrah alimsikia Mtume (saww) akisema: “Kwangu mimi watakuwepo Maamir kumi na mbili.” Jabir akaongeza kwamba Mtume alisema kitu (kwa sauti ya chini) ambacho hakukisikia na (baadae) akamuuliza baba yake kuhusu kitu hicho, ambapo alimuam-bia kwamba Mtume aliendelea kusema kwamba: “Na wote wata-tokana na Kuraishi.”²⁹

29 Jabir Bin Samrah anasimulia: “Mimi pamoja na baba yangu tulimtembelea Mtume wa Allah (swt), na nikamsikia akisema:

²⁷. *Sahih Bukhari* Sura ya 1, uk. 151. *Sahih Muslim*, JZ. 1, uk. 178.

²⁸. *Sahih Bukhari*, Sura ya 29, uk. 548.

²⁹. *Sahih Bukhari*, Sura 29, uk. 628.

Khair-ul-Bariyyah

‘Alimradi Makhalifa Kumi na Mbili wataendelea katika imani hii ya Uislamu, hautaanguka kwenye upotofu.’ Kisha akaendelea kusema kwa sauti ya chini na sikuweza kusikia alichosema. Nikamuuliza baba yangu (baadae) na akaniambia kwamba Mtume aliendelea kusema: ‘Wote watatokana na Kureishi.’³⁰

30 Jabir Bin Samrah anasimulia kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah akisema: “Maadam Waislamu watakuwa na Viongozi na Walezi Kumi na Mbili, imani yao itaendelea.” Jabir akaendelea kusema kwamba Muhammad alisema kitu zaidi ambacho sikuweza kukisikia na nikamuuliza baba yangu (baadae) kuhusu kitu hicho, na akaniambia kwamba Mtume aliongeza kusema kwamba: “Na wote watatokana na Kuraishi.”³¹

31 Jabir Bin Samrah anasimulia kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah (swt) akisema kwamba maadam Makhalifa Kumi na Mbili wataendelea katika Uislamu, utastahiki heshima na kubakia katika mamlaka. Jabir aliendelea kusema kwamba kisha Mtume (saww) akasema kitu ambacho sikuweza kukisikia na nikamuuliza baba yangu kuhusu kitu hicho, ambaye aliniambia kwamba Mtume (saww) aliendelea kusema kwamba wote hao watatokana na Kureishi.³²

32 Amir Bin Sa’d Bin Abi Waqaas anasema kwamba aliandika barua kwa Jabir Bin Sumrah na kuituma kwake kupitia kwa mtumwa wake Naaf’a, akimuomba kwamba asimuliwe Hadithi yoyote kama amesikia kutoka kwa Mtume (saww). Jabir akaandika kumjibu: “Usiku wa Ijumaa wakati Aslami alipopigwa mawe (mpaka akafa), nilimsikia

³⁰ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 119.

³¹ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 119. *Jam’a Tirmidhi*, uk. 200. *Sunan Abi Dawud*, JZ. 2, uk. 210.

³² *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 119.

Khair-ul-Bariyyah

Mtume wa Allah (swt) Akisema: “Imani hii itaendelea daima. Itaendelea mpaka Siku ya Ufufuo au mpaka Makhalifa Kumi na Mbili ambao wote wanatokana na Kureishi watakapofariki.”³³

33 Watakuwepo Makhalifa Kumi na Mbili (miongoni mwa Waislamu).³⁴

34 Watakuwepo Viongozi Kumi na Mbili katika Uislamu kama ilivyokuwa idadi ya wajumbe miongoni mwa Wana wa Israil.³⁵

35 Mtume wa Allah (swt) aliulizwa:
“Tumejifunza jinsi ya kukutolea salaam, lakini bado hatujui jinsi ya kukutakia rehema za Allah.” Mtume (saww) akasema:

“Semeni: ‘Ewe Allah! Teremsha rehema juu ya Muhammad na juu ya kizazi cha Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na kizazi cha Ibrahim. Ewe Allah! Mbariki Muhammad na kizazi cha Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahim na kizazi cha Ibrahim. Hakika, Wewe ni Mwenye kuhimidiwa na Mtukufu!’”³⁶

36 Hakuna Swala itakayokubaliwa na Allah, mpaka mtu anayeswali amswalie Mtume na kizazi chake (kama swalawati iliyooneshwa hapo juu).³⁷

³³ *Sahihi Muslim*. JZ. 2, uk. 119.

³⁴ *Mishkat* JZ. 8, uk. 93.

³⁵ *Mustadrak* JZ. 4, uk. 501.

³⁶ *Sahih, Bukhari*, Sura ya 19, uk. 305 na Sura ya 26, uk. 5. *Jam’a Tirmidhi* uk. 66 na uk. 895. *Suna Ibn Majah* uk. 65. *Sunan Nasa’i*, JZ. 1, uk. 189.

³⁷ *Jam’a Saghir*, uk. 14. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal* JZ. 2, uk. 6.

Khair-ul-Bariyyah

37 Hadharat Aisha anasimulia: “Siku moja Mtume wa Allah alitoka nje, akiwa amejifunika shuka nyeusi ya sufi. Wakati uleule akatokea Hasan Ibn Ali na Mtume akamchukua ndani ya shuka. Punde tu akafuatiwa na Husein na yeye vilevile alichukuliwa ndani ya shuka. Baada ya Husein akaja Fatima, pia naye Mtume akamchukua ndani ya shuka...mwishowe akaja Ali, naye pia Mtume akamchukua ndani ya shuka. Kwa mara moja akasoma Aya ya *Tat’hir* (utakaso):

﴿ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴾

“...Hakika Allah anataka kuwaondolea uchafu enyi Ahlu’l-Bayt na kuwatakaseni kwa utakaso kamili...” (33:33) ³⁸

38 Amr Ibn Abi Salma ambaye alilelewa na Mtume, anasema: “Mtume wa Allah (swt) alikuwa ndani ya nyumba ya Ummu Salma wakati iliposhuka kwake aya: ‘**...Hakika Allah anataka kuwaondolea uchafu enyi Ahlu’l-Bayt na kuwatakaseni kwa utakaso kamili...**’ Kisha Mtume akamchukua Fatima, Hasan na Husein ndani ya shuka na kwa vile Ali alikuwa amesimama nyuma yao, Mtume alimchukua pia ndani ya shuka na akatamka: ‘Ewe Allah! Hawa peke yao ndio hufanya kizazi changu, waondolee uchafu wa kila aina na uwatakase na utakaso kamili.’ Katika hili Ummu Salma akasema: ‘Ewe Mtume wa Allah! Na mimi niko pamoja nao?’

‘Mtume akajibu: Wewe uko kwenye nafasi yako, bakia ulipo, upo kwenye kheri.’”³⁹

³⁸ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 283. *Musnad Imam Hanbal* JZ. 1, uk. 330. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk.53.

³⁹ *Jam’a Trimdhi*, uk. 393, uk. 476 na uk. 497. *Isti’ab*, JZ. 2, uk. 473. *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 188. *Usd-ul-Ghaba* JZ. 4, uk. 39. *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 260 na uk. 261. *Mustadrak*, JZ. 3, uk. 108, uk. 146 na uk. 147.

Khair-ul-Bariyyah

39 Mansur Bin Makramah anasimulia:

“Mtume (saww) alisema: ‘Fatima ni pande la nyama yangu. Yeyote mwenye kumchukiza amenichukiza na mimi pia.’”⁴⁰

40 Mtume (saww) alisema:

“Mbora wa vijana wangu katika familia yangu ni Fatima. Yeyote yule anayemfurahisha, amenifurahisha mimi pia, na yeyote yule anayemchukiza, hunichukiza na mimi pia.”⁴¹

41 Mtume (saww) alimwambia Fatima:

“Kama unakasirishwa, Allah hukasirika, na kama unakuwa na furaha, humfanya Allah kuwa furaha pia.”⁴²

42. Mtume (saww) alisema:

“Fatima ni pande langu la nyama. Yeyote yule anayemhuzunisha, hunihuzunisha mimi, na chochote kinachomuumba yeye, huniumiza mimi pia.”⁴³

43. Hadharat Aisha anasimulia:

“Fatima, bint wa Muhammad (a.s.), alimwambia Abu Bakr ampe kile ambacho amerithi kutoka katika mali ambayo alipewa na baba yake kwa utashi wa Allah Mwenyewe, (na kile ambacho hakukipata kama ngawira). Abu Bakr akakataa akisema kwamba Mtume ametamka kwamba hataacha mrithi, na mali yoyote atakayoacha baada yake

⁴⁰ *Sahih Bukhari*, Sura ya 14, uk. 390, uk. 402 na Sura ya 21, uk. 143, *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 290. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk. 96. *Jam'a Tirmidhi* uk. 475 na 476.

⁴¹ *Mustadrak*, JZ. 3, uk. 154. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk. 97.

⁴² *Mustadrak*, JZ. 3, uk. 154. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk. 97.

⁴³ Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk. 97.

Khair-ul-Bariyyah

itakuwa kwa ajili ya umma. Hili lilimkasirisha Sayyeda Fatima, na akaacha kuongea naye, na hakuongea naye mpaka alipofariki.”⁴⁴

44 Hadhrat Aisha anasimulia:

“Fatima, bint wa Mtume (saww), alituma ujumbe kwa Abu Bakr ili ampe urithi wake kutokana na mali ambayo Allah amempa Mtume huko Madina na ambayo haikuwa ngawira, na urithi wa Fadak kutoka kwa baba yake na khums kutoka Khaibar. Abu Bakr alikataa maombi yake akisema kwamba Mtume wa Allah alisema kwamba hatakuwa na mrithi, na mali yote ambayo ataiacha baada yake itakuwa kwa ajili ya umma. Hata hivyo Abu Bakr akamkatalia katakata, na kutokana na mali yote ile hakumpa hata chembe. Hili lilimkasirisha sana Sayyeda Fatima hivyo kuanzia hapo hakuongea na Abu Bakr ingawa aliishi miezi sita baada ya Mtume. Na wakati alipofariki Ali alimzika wakati wa usiku na kumfanyia ibada zote za mazishi yeye mwenyewe, na wala hakumjulisha Abu Bakr kuhusu kifo chake.”⁴⁵

⁴⁴ *Sahih Bukhari*, Sura ya 12, uk. 140, Sura ya 27, uk. 291.

⁴⁵ *Sahih Bukhari*, Sura ya 17. *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 2, uk. 91.

Madai ya watoto wa Hadhrat Fatima yalikubaliwa kiasi ya miaka tisini baadae wakati Khalifa Umar Bin Abdul Aziz alipoirudisha Fadak kwa Imam Muhammad Baqir. Tazama kitabu “*Ma’jumul Buldan*,” JZ. 6, uk. 343, cha Yaqub Hamawi. Vilevile tazama *Ibn Athir*, *Tabari*, *Suyuti* nk.

Imesimuliwa na Ibn Jauzi kwamba hatimaye Abu Bakr aliandika hati ya kumpa haki Fatima. Hata hivyo, Hadhrat Umar kwa bahati aliwasili hapo na akauliza: ‘Kuna nini?’ Hadharat Abu Bakr akajibu kwamba ameandika hati ambayo kwayo amempa Hadharat Fatima kile ambacho Mtume amemuachia katika urithi wake. Hadharat Umar akaguta: “Kutoka kwenye chanzo gani utatumia kwa ajili ya Waislamu wakati ambapo unajua kwamba Waarabu wanajitayarisha kukupiga vita?” Wakati akisema haya aliinyakuwa hati ile (kutoka kwa Abu Bakr) na kuipasua. Tazama kitabu: “*Siratul-Halabiyah*” Jz.3, uk.346.

Khair-ul-Bariyyah

45 Abu Sa'id Khudri anasimulia:

“Wakati Aya (59:7) iliposhuka, ambayo inamwamrisha Mtume kuwapa ndugu wa karibu chochote kile ambacho ni haki yao, Mjumbe wa Allah (swt) akamwambia Fatima: ‘Ewe Fatima! Fadak ni yako.’”⁴⁶

46 Jabir Ibn Abdullah anasimulia:

“Mjumbe wa Allah aliniambia kwamba, hakika atanipa kiasi fulani, kiasi fulani na kiasi fulani cha ngawira ambacho kitakuja kutoka Bahrein. Lakini hakuna kilichopatikana kutoka huko muda wote alioishi. Wakati vitu vilipokuja baada yake, Abu Bakr alituma mpiga mbiu atangaze kwamba mtu yeyote anayemdai Mtume au aliyeahidiwa kitu naye anaweza akamfuata (ili ampatie).

“Nilimwendea Abu Bakr na kumwambia kwamba Mjumbe wa Allah aliniahidi kiasi hiki, kiasi hiki na kiasi hiki kutoka kwenye vitu vitakavyokuja kutoka Bahrein. Abu Bakr akanipa baadhi ya vitu nilivyoahidiwa. Baada ya hapo nilikwenda na kutoa madai yangu, lakini alikataa. Nilikwenda tena kwake, akakataa tena. Nilimfuata tena mara nyingine, lakini tena alikataa madai yangu. Katika hili nililalamika, ‘Nilikuja kwako mara nyingi sana bila mafanikio. Imma unipe kile ambacho ni changu au uwe kama bahili.’ Akajibu: ‘Unasema kwamba nimekutendea kama bahili. Hakuna kitu kibaya mno kama hicho.’ Na akasema hivyo mara tatu na akaendelea: ‘Kamwe sijafikiria kukunyima. Bali, kwa ndani nilikusudia kukupa (madai yako).’”

Amr alimsikia Muhammad Bin Ali akisema: “Jabir aliniambia: ‘Wakati nilipomuendea Abu Bakr (kwa mara ya mwisho), alinipa kiasi cha sarafu 500, na akaniambia atanipa mara mbili ya kisi hicho

⁴⁶ Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal* JZ. 1, uk. 228.

Khair-ul-Bariyyah

baadae.”⁴⁷

47 Anas anasimulia kwamba Mjumbe wa Allah alisema: “Baadhi ya masahaba wangu watanjia kwenye Bwawa la Kauthar. Wakati nitakapowatambua watakuwa na wasiwasi katika uwepo wangu. Kwa hiyo, nitasema kumwambia Allah: ‘Ewe Mola wangu! Hawa walikuwa masahaba wangu, na jibu lake litakuwa: ‘Hujui uzushi walioufanya katika dini baada yako.’”⁴⁸

48 Kupitia njia nyingine ya wasimuliaji inasemwa kutoka kwa Abu Hureira kwamba Mtume wa Allah alisema: “Katika Siku ya Hukumu watanjia kundi la masahaba wangu ambao watafukuziwa mbali kutoka kwenye Bwawa la Kauthar. Nitamwambia Allah: ‘Ewe Mola wangu! Hao walikuwa ni masahaba wangu.’ Na Allah atajibu: ‘Ewe Mjumbe wangu! Hujui ni uzushi gani wameufanya katika dini baada yako; wamekuwa wenye kukanusha na wamerudi nyuma kutoka kwenye Imani.’”⁴⁹

49 Amr Bin Sa’d Bin Abi Waqaas anasimulia:

“Mu’awiyah aliamwamrisha baba yangu amlaani Ali. Alikataa. Kwa hili Mu’awiyah aliuliza: ‘Ni kitu gani kinakuzuia kumlaani Ali?’ Sa’d akajibu: ‘Kwa vile ninakumbuka mambo matatu niliyoyasikia kutoka kwa Mtume ya kumsifia Ali, siwezi kujiingiza katika kumlaani Ali. Kama ningepata katika hadhi yangu moja ya sifa hizo tatu, ningependelea zaidi kuliko kuwa na msururu wa ngamia wekundu.’”

Mimi mwenyewe (yaani, Amr Bin Sa’d) nilimsikia Mjumbe wa Allah (swt) akisema kuhusu Ali wakati alipokuwa anataka kwenda vitani na

⁴⁷ *Sahih Bukhari*, Sura ya 10, uk. 54 na uk. 573, Sura ya 17, uk. 18.

⁴⁸ *Sahih Bukhari*, sehemu ya 4, uk. 97.

⁴⁹ *Ibid.* uk. 96.

Khair-ul-Bariyyah

akamuacha Ali katika nafasi yake, ambapo (Ali) aliuliza iwapo ameachwa kwa ajili ya kuwaangalia wanawake na watoto. Mtume akamwambia: “Je, huridhiki na ukweli kwamba wewe kwangu ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa, isipokuwa hakuna mtume baada yangu?”

Katika siku ya vita vya Khaibar, nilimsikia Mtume akisema: “Kesho nitampa Bendera mtu ambaye ni rafiki wa Allah na Mjumbe Wake, na pia Allah na Mjumbe Wake ni rafiki yao.” Kutokana na kauli hii (kesho yake asubuhi) tulinyoosha shingo zetu ili Mjumbe wa Allah atuone. Lakini alisema: “Niitieni Ali.” Na Ali alitafutwa. Ingawa alikuwa akiumwa macho, Mtume alimkabidhi Bendera, akatema mate kutoka mdomoni mwake na kuyaweka kwenye macho ya Ali, na katika mikono ya Ali Allah akaleta ushindi.

Iliposhuka Aya ya Mubahila (Qur’ani, 3:61) Mtume aliagiza Ali, Fatima, Hasan na Husein waitwe, na akasema: “Ewe Allah! Hawa ni kizazi changu.”⁵⁰

50. Inasimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas kwamba alisema Mjumbe wa Allah aliswali swala ya Adhuhuri na Alasiri pamoja na pia swala ya Magharibi na Isha ingawa hakuwa katika hali ya hofu wala safarini.⁵¹

51. Ibn Abbas anasimulia kwamba Mjumbe wa Allah aliswali swala ya Adhuhuri na Alasiri kwa pamoja na pia aliswali swala ya Magharibi na Isha kwa pamoja ingawa hakuwa katika hali ya hofu wala sababu nyingine yoyote, kama vile mvua. Imesimuliwa kutoka kwa Waki’i kwamba alimuuliza Ibn Abbas sababu (ya kukusanya swala). Ibn Abbas akajibu: “Ili wafuasi wasije wakaona uzito na

⁵⁰ *Sahih Muslim*, JZ. 2, uk. 278.

⁵¹ *Ibid.* JZ. 1, uk. 264.

Khair-ul-Bariyyah

shida.”⁵²

52 Abdillāh Bin Shaqī’iq anasimulia kwamba siku moja baada ya swala ya Alasiri Ibn Abbas alianza kutoa hutuba ambayo ilikuwa ndefu sana mpaka jua likazama na nyota zikatokeza. Watu walianza kupiga kelele: “Swala! Swala! (ilikuwa ni wakati wa swala ya Magharibi). Ibn Abbas hakuwasikiliza mpaka mtu mmoja kutoka Bani Tamim aliposimama na akapiga kelele kwa nguvu: “Swala! Swala!” Ibn Abbas akasema: “Ole wako! Unataka kunifundisha mimi hadithi!” aliendelea kusema: “Mimi mwenyewe binafsi nimemuona Mjumbe wa Allah akiswali swala ya Adhuhuri na Alasiri kwa pamoja na swala ya Magharibi na Isha kwa pamoja.”

Msimuliaji anasema: “Kauli hii ya Ibn Abbas ilinisumbua akilini mwangu mpaka nikaenda kumuuliza Abu Huraira kuhusu suala hilo, na akathibitisha kile alichosema Ibn Abbas.”⁵³

53 Imesimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas kwamba katika wakati mmoja Mjumbe wa Allah (swt) aliswali rakaā saba na katika wakati mwingine akaswali rakaā nane kwa pamoja. Yaani aliswali Magharibi na Isha kwa pamoja, na Adhuhuri na Alasiri kwa pamoja.⁵⁴

54 Imesimuliwa na Ibn Abbas kwamba akiwa mjini Madina Mjumbe wa Allah (swt) alikuwa akiswali swala mbili kwa pamoja (Adhuhuri na Alasiri na Magharibi na Isha) bila ya kuwepo hofu yoyote au mvua. Alipoulizwa sababu ya kufanya hivyo, alisema: “Mtume alitaka kwamba wafuasi wake wasije wakaona uzito na kwa hiyo swala mbili zinaweza kuswaliwa kwa pamoja.”⁵⁵

⁵² Ibid. JZ. 1, uk. 265. *Jam’a Tirmidhi*, uk. 54.

⁵³ Ibid. JZ. 1, uk. 265.

⁵⁴ *Sahih Bukhari*, sehemu ya 1, uk. 72.

⁵⁵ *Sunan Nasa’i* uk. 290.

Khair-ul-Bariyyah

55. Sa'id Bin Musayyab anasimulia:

“Al'Asqalaan aliibua mtafaruku kati ya Ali na Uthman kuhusiana na Muta'h (ndoa ya muda). Ali akasema kwa kupinga: 'Unataka kuwazuia watu, Ewe Uthman, kitu ambacho Mtume aliruhusu?' Uthman akajibu: 'Wacha iwe hivyo!’”⁵⁶

56 Imesimuliwa kutoka kwa Abu Nazrah:

“Nilikuwa nimekaa na Jabir Ibn Abdullah wakati alipokuja mtu mmoja na akamwambia Jabir kwamba Ibn Zubeir na Ibn Abbas walikuwa katika mabishano kuhusu Muta'h mbili, ile ya Hija na ya wanawake. Jabir akasema katika uhai wa Mtume yeye mwenyewe alizifanya Muta'h hizo mbili, lakini Umar wakati wa ukhalifa wake alizipiga marufuku.”⁵⁷

57 Abu Dharr anasimulia: “Wakati wa uhai wa Muhammad (saww) tuliruhusiwa kufanya ndoa ya Muta'h.”⁵⁸

58 Mtu mmoja alimuuliza Sa'd Bin Abi Waqaas kuhusu Muta'h, iwapo iliruhusiwa au la. Akajibu: “Tuliifanya katika wakati ambapo Mu'awiyah bado kijana mdogo.”⁵⁹

59 Umar Ibn Hasin anasimulia: “Wakati wa uhai wa Mtume wa Allah, tulifanya Muta'h, na mpaka mwisho wa uhai wake hakukuwepo na amri dhidi ya Muta'h iliyokuja juu yake, lakini mtu mmoja (Umar) alifanya alivyotaka kwa mujibu wa rai yake mwenyewe.”⁶⁰

⁵⁶ *Sahih Bukhari*, Sura ya 6, uk. 93. *Sahihi Muslim*, JZ. 1, uk. 402.

⁵⁷ *Sahih Muslim*, JZ. uk. 451.

⁵⁸ *Ibid.* JZ. 1, uk. 402.

⁵⁹ *Ibid.*

⁶⁰ *Ibid.*, uk. 403.

Khair-ul-Bariyyah

60 Jabir anasimulia: “Kwa muda mrefu tulikuwa tukifanya Muta’h kwa ukafi wa tende au unga. Wakati wa uhai wa Muhammad (saww) na pia wakati wa ukhalifa wa Abu Bakr Muta’h ilikuwa ikifanyika, lakini Umar akaipiga marufuku.”⁶¹

61 Abu Sa’id alikuwa akisimulia kwamba alimuona Mtume akifanya sijda juu ya tope, kiasi kwamba aliweza kuona alama ya tope juu ya paji lake la uso.⁶²

62 Mtume (saww) alikuwa akiweka paji lake la uso juu ya ardhi wakati akisujudu.⁶³

63 Mtume (saww) alikuwa akifanya sijda yake juu ya “*Khumrah*” (kipande cha mkeka).⁶⁴

64 Mtume (saww) alisema kwamba sehemu bora ya kusujudia ni juu ya ardhi au kile kinachoota juu yake.⁶⁵

65 Mtume alimwambia mke wake Ummu Salma: “Tafadhali niletee *Khumra* kutoka msikitini.” *Khumra* ni kipande kidogo kilichosukwa kwa makuti ya mtende ambacho ni paji la uso tu ndilo huweza kuenea wakati wa kusujudu. Ibn Athir katika kitabu chake: “*Jam’a-ul-Usul*” ameandika: “*Khumrah* ni kitu ambacho juu yake Shi’ah wa wakati wetu hufanya sijda juu yake, nakiri kwamba kwa hadithi hii ni Sunnah mtu kuiweka (na kuwa nayo

⁶¹ Ibid, uk. 451.

⁶² *Sahih Bukhari*, sehemu ya 1, uk. 104.

⁶³ Ibid uk. 97,

⁶⁴ Ibid, seh. 2, uk. 214 na 243, *Jam’a Tirmidhi*, uk. 46. *Kanz-ul-Ummal*, seh. 2, uk. 12.

⁶⁵ *Kanz-ul-Ummal*, seh. 4, uk. 113

Khair-ul-Bariyyah

wakati wote). Wale wanaoikataza na kuita kuwa ni njia ya Rafidhi wanakosea. Ili kutekeleza Sunnah hii siku zote hufanya sijda yangu juu ya kipande cha mkeka kilichotengenezwa kwa makuti ya mtende na huwa sijali upinzani wa wajinga. Tunahusika tu na Sunnah ya Mtume bila kujali iwapo wanaiita kuwa ni njia ya Rafidhi au Khawariji. Waachie tu wapayuke.”⁶⁶

66 Abdullah Bin Yusuf alinisimulia kwamba Ibn Shehad alisikia kutoka kwa Hamid Bin Abdul Rahman ambaye anasimulia kama alivyosikia kutoka kwa Abu Hureira kwamba ni kutoka kwa Mjumbe wa Allah (swt). Alisema: “Yeyote yule ambaye anayesimama kwa ajili ya kuswali wakati wa usiku wa Ramadhani kwa imani na kwa ajili ya baraka za mbinguni atasamehewa madhambi yake yote ya mwanzo.”

Ibn Shehad alisema kwamba hali hiyo ilikuwa hivyo hata baada ya kifo cha Mtume. Kisha manbo yalikuwa hivyo hivyo wakati wa ukhalifa wa Abu Bakr na wakati wa mwanzo wa ukhalifa wa Umar. Kutoka kwa Ibn Shehab kutoka kwa Urwah Ibn Zubeir na kutoka kwa Abdul Rahman Ibn Abdul Qari, inasimuliwa kwamba Abdul Rahman alisema: “Usiku mmoja tulitoka nje mimi na Umar Ibn Khattab katika mwezi wa Ramadhani na tukaenda msikitini. Tukaona kwamba mtu mmoja alikuwa akiswali peke yake na mtu fulani akiswali sehemu nyingine na kikundi cha watu kinaswali nyuma yake. Umar akasema: ‘Nafikiri ingekuwa bora kama nitawafanya wote waswali nyuma ya msomaji mmoja.’ (yaani, imamu mmoja wa swala). Kisha akaliamulia jambo hilo na akawafanya wote waswali nyuma ya Ubay Bin Ka’ab. Kisha usiku mwingine nikaenda naye tena. Watu walikuwa wanaswali Tarawehe nyuma ya imamu wao. Umar akasema: ‘Hii ni

⁶⁶ Sanni Alim Maulana Vahidul Zamankhan katika *Anwar-ul-Lughat* Sura 7 uk.118.

Khair-ul-Bariyyah

bidaa nzuri, na ile (sehemu ya usiku) ambayo kwayo watu wamelala ni bora kuliko (sehemu ya usiku) ambayo kwayo wamesimama kwa ajili ya kuswali.’ Alimaanisha kwamba usiku wa mwisho ni bora kwa ajili ya swala hizo, ambapo watu wamezoea kusimama kwa ajili ya kuswali sehemu ya mwanzo ya usiku.”⁶⁷

⁶⁷ Yahya Bin Bukair alinisimulia kwamba: “Lais alinisimulia kutoka kwa Uqail kutoka kwa Ibn Shehab ambaye alisema: ‘Alinijulisha Urwah kutoka kwa Aisha ambaye alijulishwa na Mjumbe wa Allah (swt) kwamba alitoka nje usiku mmoja na alikwenda msikitini na akaswali msikitini na baadhi ya watu wakaswali pamoja naye. Asubuhi watu wakasimulia kuhusu hilo. Hivyo, katika usiku wa tatu watu wakakusanyika kwa wingi. Mtume alitoka na kwenda msikitini akaswali pamoja nao. Hata hivyo, usiku wa nne msikiti ulifurika na watu hawakuenea, lakini Mtume aliwasili alfajiri kwa ajili ya swala ya Subhi. Wakati alipomaliza kuswali swala yake ya Asubuhi aliwatubia watu. Baada ya kutamka kalimah-e-Shahadat alisema: ‘Baada ya kumshukuru Allah, hakika kuwepo kwenu hapa msikitini hakukufichika kwangu lakini nahofia kwamba inaweza ikawa wajibu kwa ajili yenu na msiweze kuutekeleza.’ Na Mtume akafariki na mambo yakabakia kama hivyo (yaani Mtume hokuswali tena pamoja na watu swala hiyo msikitini).⁶⁸

⁶⁸. Mtu mmoja alikuja kwa Sahl Bin Sa’d, sahaba wa Mtume, kumwambia kwamba Gavana wa Madina anamlaani Ali juu ya mimbari.

Sahl akauliza: “Anamuitaje Ali?”

“Abu Turab,” akajibu yule mtu. Sahl akaangua kicheko na akasema:

⁶⁷ *Sahih Bukhari, Kitabus-Siyaam*, Hadithi Na. 1875.

⁶⁸ *Ibid.* Hadithi Na. 1876.

Khair-ul-Bariyyah

“Kwa Jina la Allah, jina hilo kapewa na Mtume mwenyewe ambalo kwalo yeye lilikuwa lenye thamani sana kuliko majina yake mengine.”

Kwa hili mtu yule alimuuliza Sahl kumueleza ilikuwaje Ali akapata jina hilo, na Sahl akaeleza:

“Siku moja Ali alitoka nje kutoka nyumbani kwa Fatima, akaingia msikitini na kujilaza chini (ya ardhi). Muda huohuo Mtume aliingia kwa Fatima na kumuulizia Ali. Fatima akamwambia Mtume kwamba Ali ameelekea msikitini. Mtume alipokwenda msikitini, akaona kwamba mavumbi yameenea mgongoni mwa Ali. Wakati anakaa ili amundoe vumbi lile, Mtume akasema: ‘Simama, Ewe Abu Turab!’”⁶⁹

69 Mtume alichinja mnyama kama dhabihu na akamfanya Ali mshirika wake katika kuitoa kama sadaka. Kisha akaamuru igawanywe.⁷⁰

70 Sa’d Bin Ubaidah anasimulia:

“Mtu mmoja alimtembelea Abdullah Bin Umar na kamuuliza kuhusu Ali. Abdullah akamuelezea sifa halisi za tabia ya Ali, na huku akioneshwa, alisema: ‘Tazama kule! Ile ni nyumba ya Ali, pale katikati kabisa ya nyumba za Mtume!’

“Lakini alipoona kwamba mtu yule hakulitaka hilo, Ibn Umar akasema baada ya kutulia kidogo: ‘Inaonekana hilitaki hilo?’

⁶⁹ *Sahih Bukhari*, Sura 2, uk. 266. Sura 14, uk. 386, Sura 25, uk. 817 na Sura 26, uk. 70. *Kunuz-ul-Haqaique* uk. 61. *Isti’ab*, JZ. 2, uk. 48. *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 154.

⁷⁰ *Ibid*, Sura ya 9, uk. 427.

Khair-ul-Bariyyah

‘Hakika, hilo silitaki,’ alisema yule mtu.

Abdullah akaguta: ‘Basi, hakika kweli Allah ameivuta pua yako nje ya kiungio. Ondoka nenda zako! Fanya utakachoweza kwa Ali!’”⁷¹

71. Abu Sa’aid Al-Khudri anasimulia:

“Tulikuwa tumekaa na Mtume wa Allah ambaye alikuwa anagawa baadhi ya ngawira wakati alipokuja Zul Khuwaisarah wa kabila la Bani Tamim na akamlalamikia Mtume - akasema: ‘Usitufanyie dhuluma!’ Mtume akajibu: ‘Nenda zako kwa shetani, kama mimi sitakuwa mwadilifu, ni nani mwingine atakuwa hivyo?’

Umar aliomba ruhusa ya Mtume ili amkate kichwa mtu yule, lakini Mtume alimkataza, akisema: ‘Mwache aende zake. Wako wengi kama yeye ambao swala zao zitadogesha swala zako wewe mwenyewe, na ambao saumu zao zitapuuzisha saumu zako wewe mwenyewe. Na Qur’ani wanayoisoma kwa makini haifiki chini kwenye koo zao. Watatoweka kutoka kwenye imani zao kama mshale unavyopenya kwenye mnyama (awindwaye). Kama alama yao, watakuwa naye miongoni mwao mtu, mweusi, akiwa na mkono kama chuchu ya ziwa la mwanamke ambao daima utakuwa unatetemeka kama pande la nyama. Watu hawa watajitokeza wakati Waislamu watakapokuwa wamegawanyika katika kambi mbili za upinzani.’

“Nashuhudia kwamba nilimsikia Mtume akitabiri yote haya. Pia nashuhudia kwamba watu hawa walipandisha hasira zao mbaya ili kupigana dhidi ya Ali ambaye kwamba nilikuwa upande wake. Ali aliamuru msako ufanywe kumtafuta mtu ambaye Mjumbe wa Allah (swt) alimtabiri. Na wakati alipoletwa mbele ya Ali, nilishuhudia

⁷¹. *Sahih Bukhari*, Sura ya 14, uk. 387.

Khair-ul-Bariyyah

kwamba alikuwa kama Mtume alivyotabiri kuhusu yeye.”⁷²

72. Zayd Bin Arqam anasimulia: “Ali alikuwa wa mwanzo kuukubali Uislamu.”⁷³

73 Ali amewatangulia wote katika kumpokea Mtume Muhammad (saww).⁷⁴

74. Miongoni mwa watu, wa mwanzo kabisa kuamini juu ya Allah na Muhammad alikuwa Ali Ibn Abi Talib.⁷⁵

75. Ali atakuwa wa mwanzo kuwasili kwa Muhammad (saww) katika Bwawa la Kauthar, akiwa yeye ni wa kwanza kuukubali Uislamu.⁷⁶

76. Imesimuliwa kutoka kwa Salman, Abu Dharr, Miqdad, Jabir, Abu Sa’id Al-Khudri na Zayd Bin Arqam kwamba Ali alikuwa wa kwanza kuukubali Uislamu, na hawa (masahaba wa Mtume) humchukulia Ali kwa heshima kubwa kuliko wengine.⁷⁷

⁷² *Sahih Bukhari*, Sura 4, uk. 343 na Sura 12, uk. 226. *Sahih Muslim*, JZ. 1, uk.431.

⁷³ *Jam’a Tirmidhi*, uk. 462.

⁷⁴ *Jam’a Saghir*, uk. 31.

⁷⁵ *Isti’ab*, Jz. 2, uk, 470.

⁷⁶ *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 155. *Isti’ab*, JZ. 2, uk. 470. *Usd-ul-Ghaba*, JZ. 2, uk. 14. *Izalat-ul-Khifa*, *Maqsad* ya 2, uk. 261. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal* uk.33.

⁷⁷ *Riaz-un-Nazarah* Jz. 2, uk. 157. *Isti’ab*, JZ. 2, uk. 470. *Tabaqat Ibn Sa’d*, Jz. 3, uk. 251. *Usd-ul-Ghaba* Jz. 4, uk. 16. *Izalat-ul-Khifa*, *Maqsad* ya 2, uk. 251.

Khair-ul-Bariyyah

77 Imesimuliwa kutoka kwa Anas Bin Malik: “Siku ya Jumatatu Mtume alipokea ujumbe wa kufikisha Uislamu, na siku iliyofuatia ya Jumanne, Ali aliswali swala zake pamoja naye.”⁷⁸

78 Ibn Afiif Kindi anasimulia: “Nilikuwa mchuuzi. Siku moja nilikwenda kuhiji Makka. Vilevile nilimtembelea Abbas Ibn Muttalib, kwa madhumuni ya kununua baadhi ya bidhaa kwa biashara, yeye mwenyewe pia akiwa ni mchuuzi. Naapa kwa jina la Allah wakati nilipokaa pamoja naye huko Mina, nilishuhudia mtu mmoja akitoka nje ya hema akichukua mwelekeo wa jua. Alipoona kwamba jua limegeuka, alianza kuswali. Wakati huohuo akatokeza mwanamke kutoka kwenye hema lilelile, na yeye pia akasimama nyuma ya mwanaume yule, akaanza kuswali. Tena, kutoka katika hema lilelile akajitokeza kijana mwenye umri mdogo, yeye pia alisimama nao akaanza kuswali. Nikamuuliza Abbas: ‘ni nani huyu?’ Abbas akajibu: ‘Ni mpwa wangu, Muhammad Bin Abdullah Bin Abdul Muttalib.’ ‘Na yule mwanamke?’ Niliuza. Akajibu: ‘Ni mke wake, Khadija Bint Khuwaylid,’ ‘na yule kijana? Akajibu: ‘Ni binamu ya Muhammad wa kwanza Ali Ibn Abi Talib.’ Nilimuuliza: ‘anafanya nini hapa?’ Akajibu: ‘Anaswali. Hujita mwenyewe ni Mtume wa Allah, lakini mpaka sasa hakuna mtu aliyemuamini isipokuwa mke wake na binamu yake. Anatabiri kwamba milango ya hazina ya Xerxes (siza) na Caesar (Kaisar) itafunguliwa kwa ajili yake.’”

Ibn Afiif ambaye aliukubali Uislamu siku chache baadaye, anasema: “Kama ningekubali Uislamu siku ileile, ningekuwa Mwisamu wa pili baada ya Ali.”⁷⁹

⁷⁸ *Jam'a Tirmidhi*, uk. 463. *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 458. *Isti'ab*, JZ. 2, uk. 472. *Usd-ul-Ghaba*, (Tarjuma) JZ. 7, uk. 22.

⁷⁹ *Riz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 158. *Usd-ul-Ghaba* (Tarjuma), JZ. 7, uk. 24. *Isti'ab*, JZ. 2, uk. 872. *Khasa'is Nasa'i* uk. 3. *Musnad Imam Hambal*, JZ. 2, uk. 209.

Khair-ul-Bariyyah

79. Mtu mmoja alimuuliza Katham Ibn Abbas: “Ilikuaje Ali akawa mrithi wa Mtume wakati wewe mwenye haki yako mwenyewe ulikuwepo pale?” Katham akajibu: “Kwa sababu kwanza aliambatana na Muhammad, na vilevile alisimama wakati wote pamoja na Mtume katika mazito na mepesi kwa nguvu zake zote.”⁸⁰

80 Ali anazo sifa nne ambazo hakuna mtu yeyote awezaye kuzifikia. Kwa wote miongoni mwa Waarabu na wasiokuwa Waarabu, alikuwa wa kwanza kuswali na Mtume wa Allah (swt), katika kila vita alipata heshima ya kukabidhiwa bendera, wakati masahaba wengine walipokimbia yeye alibakia na Mtume na ni yeye aliyemkosha Mtume na kumlaza kaburini mwake.⁸¹

81 Ni katika makubaliano ya wanachuoni wachamungu kwamba, Ali aliswali swala zake kuelekea sehemu zote, Kaaba na Baitul-Muqaddas.⁸²

82 Mtume wa Allah (swt) alisema katika nyakati mbalimbali kwamba:

“Ewe Ali! Wewe ni wa kwanza kuniamini mimi na kunivumilia.”⁸³

⁸⁰ *Mustadrak*, JZ. 3, uk. 125. *Izalat-ul-Khifa* (Tarjuma), *Maqsad* ya 2, uk. 266.

⁸¹ *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 1, uk. 202. *Izalat-ul-Khifa* (Tarjuma), *Maqsad* ya 2, uk. 261. *Isti'ab* JZ. 2, uk. 470.

⁸² *Isti'ab* JZ. 2, uk. 472. *Usd-ul-Gbaba*, JZ. 4, uk. 16. *Isabah* JZ. 4, uk. 269. *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 212. *Tabaqat Ibn Sa'd*, JZ. 3, *Qism* 1, uk. 14.

⁸³ *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 157.

Khair-ul-Bariyyah

83 Mtume (saww) alisema: “Ewe Ali! Umewazidi waumini wote nawe ni wa mwanzo kabisa miongoni mwa Waislamu kuukubali Uislamu. Wewe kwangu mimi uko kama Harun alivyokuwa kwa Musa.”⁸⁴

84 Mtume alisema (saw): “Miongoni mwenu ambaye atawasili kwanza kwenye Bwawa la Kauthar ni yule ambaye alikuwa wa kwanza kuukubali Uislamu.”⁸⁵

85 Mtume (saww) anasema: “Alikuwa ni Ali ambaye kwanza aliswali swala zake pamoja na mimi.”⁸⁶

86 Mtume (saww) alimwambia Fatima: “Je huridhii kwamba nimekuoza kwa mtu ambaye alikuwa wa kwanza kuukubali Uislamu miongoni mwa wafuasi wangu? ...”⁸⁷

87 Mtume (saww) anasema: “Watu watatu tu ndio waliokuwa watan-gulizi (katika kuamini): Joshua Bin Nun ambaye alikuwa wa mwanzo kabisa kuamini kwa Musa; Sahabe Yasin ambaye alikuwa wa kwanza kabisa kuamini kwa Isa na Ali ambaye aliwapita wengine wote katika imani juu yangu mimi.”⁸⁸

88 Ali alisema: “Miaka saba kabla ya watu hawajaanza kuswali swala zao, mimi nilikuwa nimekwishaanza kuswali swala zangu.”⁸⁹

⁸⁴ Ibid. uk. 157 na 163.

⁸⁵ *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 261. *Isti'ab JZ.* 2, uk. 470.

⁸⁶ *Kanz-ul-Haqaique*, uk. 71.

⁸⁷ *Musnad Imam Hanbal JZ.* 5, uk.26. Dondoo kutoka kwa *Kanz-ulUmmal* uk. 30.

⁸⁸ *Riaz-un-Nazarah, JZ.* 2, uk. 158. Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk. 30.

⁸⁹ *Sunan Ibn Majah* uk.12. *Riaz-un-Nazarah, JZ.* 2, uk. 158. *Usd-ul-Ghaba JZ.* 4, uk 71. *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 252.

Khair-ul-Bariyyah

89 Ali alisema: “Nilikuwa wa kwanza miongoni mwa Waarabu na wasio Waarabu kuswali pamoja na Mjumbe wa Allah (swt).”⁹⁰

90. Ali alisema: Mimi ni Mkweli Mkuu “*Siddiq Akbar*,” kwa vile nilishahadia mapema kabla ya Abu Bakr, na kabla yake niliukubali Uislamu.”⁹¹

91. Shairi (la Imamu Ali): Niliukubali Uislamu mapema kuliko wengine wote. Bado nilikuwa sijafikia utu uzima wakati huo, bali nilikuwa kijana mdogo.”⁹²

92 Amr Bin Maimun anasimulia:

“Nilikuwa nimekaa na Abdullah Ibn Abbas wakati walipokuja watu tisa wakamtaka kwamba amma wakae kando au awaambie watu wengine waondeke awe peke yake kwa vile wanataka kuongea naye kwa faragha. Ibn Abbas akaamua kutoka nje pamoja nao. Mpaka hapo alikuwa bado hajawa na matatizo na macho yake, alikuwa anaona vizuri. Mara walipotoka nje walianza mazungumzo na Ibn Abbas, na Allah anajua walichozungumza. Lakini, ghafla alirudi, akiwa amejitenga nao, na huku akikung’uta vumbi kutoka kwenye nguo zake akisema: “Wote waondoke zao kwa ajili ya lugha chafu waliyokuwa wakiitumia kwa mtu ambaye ana sifa sio chini ya kumi ambazo haku-na ambaye anazo sifa hizo, na mazungumzo yao yamejaa laana kwa yule ambaye kwaye Mtume amesema: ‘Mtu anayeweza kupewa dhamana ya kuihubiri *Suratul-Bara’at* ni mtu yule anayetokana na mimi na mimi kutokana naye.’ Siku moja Mtume aliwahutubi ami zake: ‘Ni nani miongoni mwenu anataka kuwa msaidizi wangu katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao?’ Wakati wote walipokataa, Ali

⁹⁰ *Riaz-un-Nazrah*, JZ. 2, uk. 158.

⁹¹ Ibid. uk. 157.

⁹² Dondoo kutoka *Kanz-ul-Ummal*, uk. 40.

Khair-ul-Bariyyah

akajibu: ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi ni msaidizi wako katika ulimwengu huu na ujao.’ Katika hili, Mtume akatangaza: ‘Wewe ni msaidizi wangu katika ulimwengu huu na ujao.’ Kisha, akiwa amemuweka Ali kando, Mtume akarudia maneno yale tena (akiwahutubia ami zake) na akamtaja mtu mahususi. ‘Ni nani miongoni mwenu anataka kuwa msaidizi wangu katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao?’ Wote wakakaa kimya. Mara nyingine tena Ali akarudi: ‘Mimi ni msaidizi wako katika ulimwengu huu na ujao.’ Kwa hili Mjumbe wa Allah akamhakikishia: ‘Wewe ni msaidizi wangu katika ulimwengu huu na ujao’...’⁹³

⁹³ *Riaz-un-Nazarah*, JZ. 2, uk. 203. *Isabah* J, 4, uk. 270. *Izalat-ul-Khifa Maqsad* ya 2, uk. 252 na 261, *Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal* Jz. 1, uk. 330.

Khair-ul-Bariyyah

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia

Khair-ul-Bariyyah

26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba

Khair-ul-Bariyyah

56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume
Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia
iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira

Khair-ul-Bariyyah

84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqaalain
102. Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili

Khair-ul-Bariyyah

111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
114. Iduwa ya Kumayili.
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii

Khair-ul-Bariyyah

136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kikusunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kikusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kikusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini Swala ya Jamaa.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya kwanza

Khair-ul-Bariyyah

160. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya Pili
161. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
162. Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Huduma ya Afya katika Uislamu
164. Hukumu za Mgonjwa
165. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein
166. Uislamu Safi
167. Majlis ya Imam Husein
168. Mshumaa
169. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
170. Uislam wa Shia
171. Amali za Makka
172. Amali za Madina
173. Uislamu na mfumo wa Jamii ya dini nyingi
174. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
175. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
176. Elimu ya Tiba za Kiislam Matibabu ya Maimamu
177. Falsafa ya Dini

Khair-ul-Bariyyah

BACK COVER

Jina la kitabu hiki linatokana na hadithi ya Mtukufu Mtume SAW kama ilivyosimuliwa na Ibn 'Asakir kutoka kwa Jabir bin Abdallah kwamba alisema: "Tulikuwa pamoja na Mtume SAW wakati Ali AS alipokuja (hapo tulipokuwa tumekaa). Mtume akasema: 'Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake; hakika huyu (Ali) na Shia (wafuasi) wake ndio wenye kufuzu Siku ya Ufufuo.' Kisha aya ifuatayo ikashushwa: *'Hakika wale walioamini na kutenda mema, basi hao ndio wema wa viumbe!'*"

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

Khair-ul-Bariyyah
